

**Yohana Mbatizaji.** Utume mwema wa Yesu 1  
Kristo, Mwana wa Mungu, ulianza, /kama uli- 2  
vyoandikwa na mfumbuaji Yesaya: Tazama,  
mimi namtuma mjumbe wangu, akutangulie;  
naye atatengeneza njia yako. / Iko sauti ya 3  
mtu apigaye mbiu nyikani: Itengenezeni njia  
ya Bwana! Yanyoosheni mapito yake!

Yohana Mbatizaji alikuwa nyikani akibati- 4  
za na kutangaza ubatizo wa kujuta, wapate  
kuondolewa makosa.